

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA**

SHULE YA SEKONDARI BANEMHI,

S.L.P 519,

**BARIADI.**

...../.../20.....

**KUMB NA. BSS/11/VOL.10/.....**

Jina la mwanafunzi.....

.....

S.L.P 399,

**BARIADI.**

**YAH; MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BANEMHI WILAYA**

**YA BARIADI VIJJINI MKOA WA SIMIYU KWA MWAKA 20.....**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Banemhi kwa mwaka 20....., shule ya sekondari ipo umbali wa km 30 kutoka makao makuu ya Halmashauri wilaya ya Bariadi.

Mhula wa masomo unaanza tarehe...../...../20.... Unatakiwa kuripoti shulen kuanzia tarehe...../.....20..... Ndani ya siku saba(7) tangu shule kufunguliwa , masomo yanayofundishwa ni

***KIINGEREZA,KIURAJA,JIOGRAFIA,HESABU,FIZIKIA,BAIOLOJIA,HISTORIA,KEMIA, na KISWAHILI.***

**2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE ZA SHULE**

**2.1.1** Suruali mbili (kijani kilichoiva na dark blue) kwa wavulana.

2.1.2. Tai mbili (kijani kilichoiva na dark blue) wavulana na wasichana.

2.1.3 Viatu vyeusi na soksi nyeusi pea mbili kwa wavulana.

2.1.4 Sketi mbili (kijani kilichoiva na dark blue) zote ziwe ndefu ziguse kisigino, kitambaa

Kitambaa kiwe kizitoi, aina ya mshono rinda moja kubwa mbele na rinda moja kubwa nyuma , pemberi ni marinda madogo matatu kila upande. Aidha mnatakiwa kuwasiliana na wanaosoma katika shule yetu ili wawape maelekezo Zaidi kuhusu mshono huo .

2.1.5. Shati 2 za mikono mifupi kwa wavulana na wasichana.

2.1.6. Sare za michezo ni Track suit ya rangi ya bluu na viatu vya michezo.

2.1.7. Daftari kubwa (counter books 10 na daftari za kawaida 10).

2.1.8. Mathematical sets(mkebe).

2.1.9. Dictionary (kamusi) ya kiingereza-kiswahili. Mambo yote haya yatakaguliwa shulenii.

### **3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.**

- i. Heshima kwa viongozi wazazi, wafanyakazi wote , wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- ii. Mahudgurio mazuri katika shughuli ndani nan je ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- iii. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- iv. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia maelekezo juu ya kuwepo ndani nan je ya mipaka hiyo wakati wote wa ufanuzi wako katilka shule hii.
- v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule hii.
- vi. Kuvala sare ya shule wakati wote inapotakiwa.
- vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
- viii. Kutunza mali za umma.

### **5.0. MAKOSA YAFUATAYO YAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AMA KUSIMAMISHWA SHULE.**

- i. Wizi.
- ii. Uasherati na ushoga.
- iii. Ubakaji.
- iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa kama vile bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
- v. Kupigana na kupiga.
- vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- vii. Kudharau bendera ya taifa.
- viii. Kupata ujauzito(mimba).
- ix. Kuoa au kuolewa.
- x. Kutoa mimba.
- xi. Kugoma , kuongoza , kushiriki au kuvuruga mani na usalama wa shulenii au watu.
- xii. Kukataa adhabu kwa makusudi.
- xiii. Kuwa na simu ya mkononi.

**NB; Mzazi/mlezi atawajibika kwa mambo yote yanayomhusu mwanae ( Matibabu, usafiri ,chakula na mengineyo).**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

.....

**ANGELA P. KAMGISHA**

**MKUU WA SHULE.**